TAARIFA YA UPANUZI WA MTAMBO WA RUVU JUU NA UJENZI WA BOMBA KUTOKA MLANDIZI HADI KWENYE MATANKI YA KIMARA NA MRADI WA UPANUZI WA MFUMO WA UGAWAJI MAJI DAR ES SALAAM NA PWANI

Ifuatayo ni tarifa fupi ya miradi ya maji inayosimamiwa na DAWASA itakayotembelewa na Waheshimiwa Wabunge wa Kamati ya Maji, Mifugo na Ardhi tarehe 20 januari 2018

Upanuzi wa mtambo wa Ruvu Juu

Upanuzi wa mtambo wa Ruvu Juu umewezesha mtambo huo kuongeza uzalishaji kutoka lita milioni 82 hadi kufikia lita mlioni 196. Mradi huu ulizinduliwa rasmi na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli Juni 21, 2017 baada ya kukamilika.

Kazi zilizofanyika ni pamoja na Ujenzi wa nyumba za wafanyakazi, Ujenzi wa maeneo ya kusafisha maji, Ujenzi wa eneo la kuchuja tope ili kuwezesha maji ghafi kutumika kwa ufanisi, Tenki la maji safi, machujio (Rapid Sand Filters). Ujenzi wa kituo cha kusukuma maji yaliyosafishwa kwenda kwa watumiaji, ujenzi wa Kituo cha kusukuma maji ghafi Ruvu darajani, Ujenzi wa njia mpya ya umeme kutoka Chalinze, Ujenzi wa kituo kipya cha kupokea umeme wa msongo mkubwa na Ufungaji wa Pampu mbalimbali. Mradi huu uligharimu dola za Marekani milioni 39.7

Ujenzi wa bomba kuu kutoka Kibaha hadi Kimara

Ili maji yaliyoongezeka yaweze kuwafikia watumiaji, mradi wa ujenzi wa mabomba makuu na tenki la Kibamba ulitekelezwa.

Katika mradi huu, kazi zifuatazo zilifanyika; Ulazaji wa mabomba jumla ya **km 69.569** yenye kipenyo cha 1200mm, 100mm na 900mm, Ujenzi wa jengo la ofisi ya mradi Kibaha ambalo hivi sasa linatumiwa katika shughuli za kuendeshea huduma za maji Kibaha, Ujenzi wa tanki lenye ujazo wa lita milioni 10 eneo la Kibamba, Ukarabati wa matanki mawili yenye ujazo wa lita milioni 8 kila moja yaliyopo Kimara Mwisho. Kuunganisha bomba jipya la 1000mm na la zamani 600mm eneo la Kimara Temboni ili kuboresha huduma ya usambazaji maji.

Mradi huu uliogharimu dola za Marekani milioni 59 nao ulizinduliwa na Mheshimiwa Rais sambamba na mradi wa upanuzi wa mtambo.

Mradi wa uboreshaji wa huduma za ugawaji na usambazaji maji katika baadhi ya maeneo ya Mikoa ya Pwani na Dar es salaam

Mradi wa uboreshaji wa huduma za ugawaji na usambazaji maji katika baadhi ya maeneo ya Mikoa ya Pwani na Dar es salaam unaendelea kutekelezwa kwa kasi katika maeneo mbalimbali jijini Dar es salaam na katika Miji ya Bagamoyo na Kibaha na tayari umefikia asilimia 72.2.

Mradi huo unaotekelezwa na Wizara ya Maji na Umwagiliaji kupitia Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Dar es salaam (DAWASA) ulianza rasmi mwezi Machi mwaka 2016 na hivi sasa unaendelea kutekelezwa katika maeneo mbalimbali.

Kazi zinazofanyika chini ya mradi huu ni pamoja na ujenzi wa matenki tisa (9) ya kuhifadhi na kusambaza maji yenye ukubwa wa kuhifadhi kati ya lita milioni 3.0 hadi lita milioni 6.0; ujenzi wa vituo vinne (4) vya kusukuma maji, ununuzi na ufungaji wa pampu kubwa za kusukuma maji 16, ununuzi wa transfoma na ufungaji njia za umeme wa msongo mkubwa, ununuzi na ulazaji wa mabomba makubwa ya ugawaji maji na ulazaji wa mabomba ya usambazaji maji mitaani yatakayokuwa na urefu wa jumla ya kilometa zipatazo 477.

Maeneo yatakayonufaika na mradi huu ni pamoja na Salasala, Bunju, Wazo, Makongo, Changanyikeni, Bagamoyo, Mpiji, Zinga, Kiromo, Kitopeni, Ukuni, Kerege, Buma, Mataya na ukanda maalum wa EPZA ambayo ni maeneo yanayohudumiwa na mtambo wa Ruvu Chini.

Maeneo mengine yatakayonufaika na mradi huu ni yale yaliyopo kati ya Mbezi Luisi na Kiluvya, ambayo ni Kiluvya, Kibamba, Mbezi, Msakuzi, Makabe, Malamba mawili na Msigani. Maeneo haya huhudumiwa na mtambo wa Ruvu Juu ambao ulizinduliwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Juni 21, 2017.

Lengo la mradi huu ni pamoja na kuhakikisha kuwa wananchi wa kawaida, wenye viwanda na biashara katika eneo lote la mradi wanatapa huduma bora za maji hasa baada ya maji kuongezeka kufuatia kukamilika kwa kazi za upanuzi wa mitambo ya maji ya Ruvu Juu na Ruvu Chini. Lengo lingine ni kuweka mitandao ya maji katika maeneo ambayo hayakuwa na mtandao rasmi wa maji; kwa kufanya hivi, mradi utawezesha maji yagawanywe kwa ufanisi na uwiano zaidi. Chini ya mradi huu, Matenki hayo mapya yanajengwa maeneo ya milimani ili kuweza kufikisha maji katika maeneo yote ambayo hayapati maji kutokana na miinuko. Chini ya mradi huo miundombinu chakavu pia itakarabatiwa, hivyo kwa ujumla huduma ya maji itakuwa bora na uhakika zaidi mradi utakapokamilika.

Ili kudhibiti upotevu wa maji, mita maalum zitafungwa katika maeneo ya kupokea maji na katika matoleo ili kujua kiasi kamili cha maji kilichoingia katika eneo husika na kiasi cha maji kitakachogawanywa kwa wananchi. Tofauti na mita za kawaida, mita hizi zitakuwa zinapeleka taarifa moja kwa moja katika ofisi za uendeshaji ambapo vifaa maalum vitafungwa na itakuwa rahisi kutambua ni wapi maji yanapotea na hivyo kuyadhibiti mara moja.

Mradi huu unatekelezwa kwa gharama ya dola za Marekani milioni 32,927,222.45 kupitia mkopo wa masharti nafuu kutoka Serikali ya India.

Imetolewa na Ofisi ya Uhusiano wa Jamii -DAWASA